102/3 - KISWAHILI- Karatasi ya 3

Fasihi

BUNAMFAN CLUSTER EXAMINATION 2022

MWONGOZO

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU A**

**USHAIRI**

**1. *Lazima***

**Monyara**

Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara
Tuliochelea kukaribia kingo zake
Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia
Kwa kunyenyekea wingi wa yake maji
Yaliyojiendea utadhani yamesimama.

Ni katika mto huu
Ambapo samaki wakubwa tulivua
Maguo kuyatakasa japo kwa kunyemelea
Na walevi stadi wakachelea kuuvuka
Ulipofura na kupita kwa kiburi
Kwa kushiba maji yake
Yaliyofanya mawimbi madogo.

Ni hapa ambapo marehemu nyanya
Mkono alinishika na njia kuniongoza
Juu ya ulalalo wa miti
Vikapu vyetu hewani vikielea;
Mimi nikishika changu kwa mkono mmoja
Naye akikiachilia chake kujishikisha kichwani
Masafa baina yetu na mtambo
Uliokwenda kwa maji
Tuliyapunguza kwa kila hatua tulopiga.

Ni katika mto huu ambapo
Samaki tuliowavua tuliwapasua na kuwasafisha
Na hivyo kuuficha umaskini wetu
Ulotuzuia kununua mnofu wa bucha
Ni hapa ambapo wanawake walifika
Mawe ya kusagia kupata
Ni katika mto huu ambapo
Waumini walifika kutakaswa kwa ubatizo
Baada ya ulevi, uzinzi na kufuru nyinginezo.

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa
Hata wachawi walifika kufanya vitimbi vyao
Baada ya utawala wa jua kumezwa na nguvu za giza
Sasa Monyara nilioijua haipo tena
Zimebaki kingo zilizokaukiana
Kama uso wa mrembo aliyekosa mafuta
Siku ayami.

Mto huu ambapo pembeni mwake
Watoto walipashwa tohara
Maji yake yakishangilia, umekonda
Na mbavu zake nje kutoa
Na sasa vitoto vikembe vinazikanyaga
Vikijiendea zao kusaga mahindi
Juu mlimani
Katika mtambo wa Kizungu
Usioisha kulalamika
Nao wanawake hawaji tena
Kutafuta mawe ya kusagia wimbi
Imebaki njia ya walevi warejeao nyumbani
Nayo miti iliyosimama wima ukingoni
Iliisha kuanguka kwa kuleweshwa na pumzi za walevi
Wasioisha kupita hapa.

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

(a) Onyesha umuhimu wa Mto Monyara kwa wanakijiji. (alama 4)

i) Kuvua **samaki** ambao watatumiwa kama kitoweo;
ii) **Nguo** zilioshewa humo;
iii) Maji yake yaliendesha **mtambo**, kinu cha kusagia unga;
iv) **Mawe** ya wanawake ya kusagia waliyapata humo;

v) Waumini wali**batizwa**/walitakaswa katika maji ya mto huo baada ya dhambi za ulevi na uzinzi;
vi) Wachawi waliutumia kufanya **vitimbi** vyao;
vii) Watoto walipashwa **tohara** kando yake, maji yalishangilia waliopashwa tohara

*(Hoja zozote 4x1= alama 4)*

(b) Toa mifano ya mishata inavyojitokeza shairini. (alama 2)

Mshororo usiokamilika, unakamilikia katika ule unaofuata.

Ni katika mto huu ambapo

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa

*(zozozte 2x1=alama2)*

*Tathmini jibu la mwanafunzi*

(c) Eleza aina **tatu** za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
i) Taswira **mwendo**: kuenda ka maji, kuuvuka mto, vitoto kuenda kusaga mahindi;
ii) Taswaira **mguso**: Mikono ya nyanya na msimulizi kushikana.
iii) Taswira **mwono**: maji kusimama, vikabu kichwani na mkononi.
*(za kwanza 3x1=3)*

(d) Fafanua mtindo katika shairi hili. (alama 3)
i) **Mbinu rejeshi**: kumbukumbu za hali ya awali yam to Monyara;
ii) **Tashihisi**: mto ulipita kwa kiburi na ulishida maji yake; mto umekonda na kutoa mbavu zake nje;
iii) **Taswira**: msimulizi na nyanya tunawaona wakishikana mikono wakivuka mto kwa kupita juu ya ulalo wa miti;
iv) **Tashibihi**: maji yalijiendea utadhani yamesimama,
v) **Utohozi**: bucha;

(e) Tambua nafsi neni ya shairi hili. (alama 1)

**Mjukuu**;

Msimulizi

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

*(Hoja1x1=1)*

(f) Jadili idhini ya kishairi katika shairi. (alama 3)
i) **Inkisari**: tulopiga- tuliyopiga Ulotuzuia-uliotuzuia;
ii) **Kuboronga** msamiati: Miundo mibaya ya sentensi, mfano, ukakamavu kujihamia- kujihami na ukakamavu, Mawe ya kusagia kupata – Kupata mawe ya kusagia
iii) **Mazda**: kujihamia- kujihami
iv) **Utohozi**: Bucha

*(zozote 3x1=alama3)*

(g) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari (alama 2)

Msimulizi anaeleza kuwa walivua samaki wakubwa *katika Mto Monyara* kabla haujakauka. Kwa kuwa maji ya mtohuo yalikuwa mengi *kutokana na kufurika*, waliogopa kuoshea nguo ndani yake na hivyo wakazioshea kando. Walevi waliokunywa pombe ng'ambo ya pili waliporejea makwao, *waliogopa kuuvuka* kutokana na wingi wa maji yake. Mto ulipofurika ulifanya mawimbi kidogo kuonyesha maji yalikuwa ya *kina kirefu*.

$(Zozote\ 4x\frac{1}{2})$

(h) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

Toni ya **kutamauka**/kukata tamaa- Mto Monyara uliowapa wenyeji matumaini ya maisha mema sasa hauko, umekauk

**SEHEMU YA B**

**Riwaya**: *Chozi la Heri* - Assumpta Matei
Jibu swali la *2 au 3*

**2.** "Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe na baadaye wanagawana ngawira nao!"

***a)***

i. Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

Msemaji: **Rachel Apondi**;
Wasemewa: vikosi vya **usalama**/walinda usalama;
Mahali: **Warsha**;
Kuhusu: **jukumu** la vikosi vya usalama, amani na maridhiano. Alikuwa akiwasuta walinda usalama ambao wanatumia ushawishi/mamlaka yao kujitajirisha kwa njia za kifisadi.)

*(Zote 4x1=alama4)*

ii. Jadili mtindo katika dondoo hili (alama 3)

i. **Kinaya**: Haitarajiwi walinda usalama kushirikiana na wezi kuiba na kisha kugawana ngawira;
ii. **Nidaa**: wanagawana ngawira nao!
iii. Nahau/**msemo**:wanagawana ngawira

iii. Eleza sifa za usemaji wa dondoo hili (alama 3)

i. Mwenye **bidii**: analea Sophie kwa juhudi;
ii. **Msomi**: Anafunza warsha;
iii. **Mkarimu**: anamkaribisha Umu. Aidha, anapokutana na Mwangeka kwa mara ya kwanza anamzungumzia vyema;
iv. **Mwajibikaji**: anaishughulikia familia vilivyo.

*(zozote 3x1)*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

***b)*** Ufisadi unaojadiliwa katika dondoo una madhara katika jamii ya Wahafidhina. Jadili. (alama 10)

i. Unasababisha **uharibifu** wa mali. Majumba makubwa ya mabwanyenye akiwemo Ridhaa yaliyojengwa kwenye arhi iliyotengewa ujenzi wa barabara yanabomolewa;
ii. Baadhi ya familia zinaachwa bila makao baaa ya majumba kwenye mtaa wa Tononokeni ku**bomolewa** ili kupanua barabara;
iii. Unapelekea viongozi wabaya pale vijana kama aliyevalia shati lililoandikwa 'Hitman' wanapohongwa **kuchaguliwa** ili kusaidia kuiba kura;
iv. Hupelekea **umaskinishaji** kwa vile mashamba madogomadogo yananyakuliwa na mabwanyenye wenye wenye mahsamba makubwa kwa mujibu wa kijana aliyevalia shati lililoandikwa 'Hitman';
v. Kupanuka kwa **mwanya** kati ya matajiri na maskini/huzidisha utabaka kwani mabwanyenye wananyakua ardhi ya maskini na kujenga viwanda na maduka ya kibiashara huku maskini wakibaki bila ardhi, kwa mujibu wa kijana aliyevalia shati lililoandikwa'Hitman';
vi. Inasababisha **ubadhirifu** wa pesa za umma kwani serikali inabuni tume za kuchunguza ufisadi na ripoti zenyewe hazionekani;
vii. Kufutwa **kazi** kwa watetezi wa haki,mfano Lunga na Shamsi wanafutwa kazi kwa kugoma;
viii. Unasababisha **mahindi** yaliyo hatari kwa usalama wa raia kuletwa nchini;
ix. Uharibifu wa **mazingira**/misitu-matrekta ya viongozi yanabeba shehena za mbao, makaa na mahindi kutoka kwenye msitu wa Mamba usiku wa manane;
x. **Uhamisho** wa lazima-viongozi wanawahamisha wananchi kutoka kwenye msitu wa Mamba ili wapate mwanya wa kunyakua malia mbayo tayari walikuwa wamezalisha;
xi. Bei ya **samaki** kupanda hasa kufuatia nani kamiliki Ziwa Kuu. Huku kunawafanya wananchi kununua bidhaa hii kwa bei ghali kwa mujibu wa Kairu;
xii. **Ukiritimba**: ni watu wachache wanaouza samaki kutokana na bei ya samaki kupanda maradufu;
xiii. Ongezeko la **wizi**/ukosefu wa usalama-polisi wanaposhirikiana na wezi kuiba na kisha kugawana ngawira;
xiv. Kuvunjwa kwa **sheria** za barabarani: polisi wenye madaraka wanapoacha magari yao makuukuu barabarani kwa kutumia ushawishi wao;
xv. Huduma mbovu/duni za **afya** kwa vile dawa zilizopaswa kuwatibu watu hospitalini zinaibwa na kupelekwa katika maduka ya wasimamizi wa hospitali;
xvi. Unywaji wa **pombe** haramu-watoto wa maskini wanajiingiza katika unywaji wa pombe haramu wanapokosa mikopo na ruzuku inapotolewa kwa wanaojiweza;
xvii. **Ulanguzi** wa dawa zakulevya-wanafunzi kutoka familia maskini wanapokosa mikopo ya ruzuku, kwa vile inatolewa kwa watoto matajiri,wanajiingiza katika ulanguzi wa dawa za kulevya ili kujipurukusha na hali duni ya masomo chuoni. Buda analainisha viganja vya maofisa wa forodha ili kueneleza ubebaji fafina;

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

xviii. **Utamaushi**- shamsi anapoteza matumaini anapokosa ajira kwa vile nafasi za ajira hutolewa kwa mapendeleo(kwa jamaa), kinasaba;

xix. **Vifo**- wanafunzi wa shahada ya uzamili wanakufa kutokana na unywaji wa dengelua wanapokosa mikopo na ruzuku inayotolewa kwa mapendeleo kwa wanafunzi wanaojiweza;

xx. Husababisha **ubaguzi** kwa sababu nafasi za ajira zinatolewa kwa mapendeleo kwa wanafunzi wanaojiweza. Shamsi anakosa ajira kwa sababu hii;

xxi. Dhiki za ki**saikolojia**-Dick anatatizika kisaikolojia Buda anapotishia kumfisha kama hatalangua mihadharati;

xxii. Hupandisha tamaa na **ubinafsi**- lunga anabadili nia yake ya kuhifadhi mazingira na kuanza kukata miti punde tu anapostaafishwa;

xxiii. Husababisha ulanguzi wa binaamu- **Sauna** na Bi Kangara wanashirikiana na wajasiriamali kulangua na kuuza watoto ughaibuni;

xxiv. Husababisha **ufuska**- Bi Kangara na Sauna wanawauza watoto wa kike katika madanguro wanakoendelezea ufuska;

xxv. Husababisha adhabu hafifu kwa wavunja **sheria**- badala ya Fumba kuachishwa kazi anarudishwa kazini na kupewa uhamisho anapofanya mapenzi na kumtia ujauzito mwanafunzi wake, Rehema;

xxvi. **Upofu**- walevi wanaokunywa dengelua ya vijasumu wanapofuka, kulingana na Shamsi.

xxvii. Ulaghai/**utapeli**- Sauna anauza maji ya mito na madimbwi anayoyatia kwenye chupa za vibandiko vya *mineral water*;

xxviii. Watu kupoteza **pesa** baada ya kuuza vipande vya ardhi vilivyotengewa makaburi.

*(zozote 13x1=alama 13)*

**3.**

***a)*** Jadili mtindo kwenye dondoo hili. (alama 8)

Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu,Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa – mwamu hasa – akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizimwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini! Wanasema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la maama, hili la mbwa ataliamwa!

*Majibu:*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

i. Taswira **oni**:jua linalochomoza halina ule wekundu;
ii. **Nahau**/msemo: wanangu wakembe, majeraha kikwi;
iii. **Ishara**: wingu kubwa angani, umeme, mtutumo;
iv. **Tashihisi**: mawingu kupiga busu, mawingu kushiba;
v. **Takriri**: siye, siye;
vi. **Tashibihi**: kuvimbiana kama donge la unga ngano;
vii. **Nidaa**: mzizi! Daktari mzima! Chini!
viii. **Methali**/mdokezo wa methali: samba akikosa nyama hula nyasi, Msafiri kafiri ati,amekosa la mama, hili la mbwa ataliamwa;
ix. **Mbinu rejeshi**; Kifungu chote ni usimulizi wa yaliyotokea.

*(zozote 8x1)*

***b)*** "Huyu hapa ni Bwana Mwangemi na huyu hapa ni Bi Neema. Kama nilivyokujuza hapo awali, wamekuja kuchukukua kwenda kuishi nao kama mwana wao."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

i. Msemaji: + Mwale;
ii. Msemewa: **Mwaliko**;
iii. Mahali: Kituo cha **Benefactor**;
iv. Kinachotokea: Anamweleza Mwaliko kuwa **atapangwa** na Neema na Mwangemi

(zozote 4x1= alama 4)

ii) Banaisha mtindo katika dondoo. (alama 3)

i. **Uashiriaji/**uigizaji: Huyu hapa ni Mwangemi na huyu hapa ni Neema'
ii. **Tashibihi**: Kuishi nao kama mwanawao;
iii. **Mbinu rejeshi**: kama ni*li*vyokujuza hapo awali;
iv. **Takriri**: 'Huyu hapa' imerudiwa.

*(zozote 3x2=alama 6)*

iii) Toa sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 5)

Sifa za Anastacia Mwale:

i. **Mwajibikaji**: atamtembelea Mwaliko mara kwa mara ajue vile anaendelea;
ii. **Mkarimu**: Anamkaribisha Mwangemi Neema;
iii. Mpenda **utaratibu**: atayarishia Mwangemi stakabahi asmi za kupanga motto huyu;
iv. Ana **kumbukumbu** nzuri: anakumbuka maelezo ya Mwaliko alimpatia;
v. Mwenye **mlahaka** mwema: anawakaribisha kina Mwangemi.

*(zozote 5x1= alama 5)*

**SEHEMU YA C**

**Tamthilia:** *Kigogo* **-** Pauline Kea

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

Jibu swali *4* au *5*

**4.** Mwandishi wa tamthilia ya *Kigogo* amefanikiwa katika kutumia ishara ili kufanikisha maudhui. (alama 20)

i) **Fimbo** ya Kenga yenye kichwa cha nyoka ni ishara ya jinsi alivyokuwa katili kwa raia;
ii) Kitendo cha Majoka cha kuzungumza na **babu** yake anapozirai ni ishara kuwa wafu walikuwa wakimwita madhali ndiye aliyekuwa amewaua;
iii) Majoka kuvaa **mkufu** shingoni wenye kidani cha umbo la swila ni ishara ya namna Majoka alivyokua hatari kwa maisha ya raia wa jimbo la Sagamoyo.
iv) **Kilio** na machozi mengi ndani ya ziwa lililofunika damu ni ishara ya raia waliouliwa na Majoka wanalilia hali yao.
v) **Kutojaa** kwa raia ilivyo kawaida katika mkutano wa kudumisha sherehe za uhuru pamoja na sikub ya kuzaliwa kwa Majoka ni ishara ya raia kuasi Majoka kutokana na uongozi wake dhalimu.
vi) Hali ya Majoka kujiona ndani ya **ziwa** lililofurika damu ni ishara ya mauaji mengi ya raia aliyokuwa akitekeleza katika uongozi wake.
vii) Damu ya **Jabali** anayoiona Majoka ikitiririka mikononi mwake akiwa amezirai ni ishari kuwa ndiye aliyemuua Jabali;
viii) **Bastola** ya Majoka (uk 38) silaha au chombo cha kuwatishia watawaliwa na watetzi wa maovu ya kiongozi yanayopendezwa.
ix) Chai ya **maziwa** (uk 31)kinywaji cha watu wenye mapato mazuri tabaka la juu.
x) Chai ya **mkandaa-**kinywaji cha watu maskiniinaonyesha utabaka.
xi) **Nyoka** (uk 31) huashiria ushirikina na ukatili wa Majoka.
xii) Chombo cha **safari** ya angani (uk 30)huashiria uongozi au madaraka.Majoka ni mojawapo wa marubaini (babu,uk 80)yaani yeye ndiye kiongozi ambaye huwalaghai anawaongoza.

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

xiii) **Embe** lililoiva kupitia kiasi (uk1)ni ishara ya kuzorota kwa uchumi wa Sagamoyo.

xiv) **Gari** la kifahari (uk 8)Hali ya utajiri wa kupindukia wa viongozi na ubepari pia utamaduni wa kizungu.
xv) **Hoteli** za kifahari (uk 67) huashiria starehe ya tabaka la juu.
xvi) **Kinyago** (uk 10) huashiria hali ya viongozi kupenda uluwa;hali ya viongozi kupenda makuu kwa kutaka majina ya watu wa mbani zao yazaidi kusifiwa milele kwa kuwa walipigania uhuru.
xvii) **Kiti** cha fahari(uk 19)huashiria tabaka la juu kiuchumi,tabaka lenye starehe kutokana na utajiri wake.
xviii) **Mbuyu** (uk 15) Mbuyu ni makao ya shetani kwa hivyo matumizi yake huashiria dhuluma za kiongozi.Kenya anawahutubia wahni dhini ya mbuyu.

xix) Mkufu wenye **kidani** cha umbo la swila (uk19)ni nembo ya uongozi wa kadhalimu ,pia isahara ya ushirikina.

xx) **Ndoto** ya Tunu(uk 53)ufunuo wa madhila ya wapiganaji/wanajamii wakati wa uongozi uliopita wa babake Majoka,Marara na bin Ngao.

xxi) **Pombe** ni ishara ya utovu wa maadili ya jamii.

xxii) Kukauka kwa **mito** na maziwa ni ishara ya kuisha kwa ushawishi wa Majoka katika Sagamoyo.

xxiii) **Redio** (uk 3)huashiria maendeleo ya kitenolojia yanayotumiwa na viongozi kujikuza wenyewe.

xxiv) **Rununu** (uk 3) ishara ya maendeleo katika uwanja wa mawasiliano.Ni kinaya kwa sababu hatuoni maendeleo haya ya kimawasiliano yakichangia kuiboresha hali ya maisha ya ,mwaananchi wa kawaida.

xxv) **Soko** chafu kuashiria ishara ya uozo wa kimaadili wa kisiasa.

xxvi) **Sumu** ya nyoka (uk4) kuashiria dawa za kulevya na masaibu yanayotokana na masaibu ya wafanyikazi wa tabaka la chini yanayotokana na kunyanyaswa na viongozi au wajiri katili.

xxvii) **Maziara** kujaa ishara ya mauaji ya watuchini ya watu chini ya utawala wa Majoka.

*(zozote 10x2=alama 20)*

**5.** Mimi sili makombo kama kelbu! Nilishakunywa chai ya mke wangu nikaridhika."

(i) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)

i. Msemaji: **Sudi**;
ii. Msemewa: **Boza** na Kombe;
iii. Mahali: **Karakana** ya uchongaji katika soko la Chapakazi;
iv. Kiini: Sudi alisusia makombo ya keki iliyoletwa na Kenga kwa kuwa alijua alikokuwa keki kubwa.

*(zote 4x1=alama 4)*

(ii) Fafanua mtindo katika dondoo hili. (alama 4)

i. **Tashibihi**: makombo ya kelbu;
ii. **Nidaa**: Mimi sili makombo kama kelbu!
iii. **Jazanda**: makombo, kelbu, chai;
iv. **Mbinu rejeshi**: Nilishakunywa chai ya mke wangu nikaridhika

(iii) Jadili vile Wanasagomoyo wamefanywa kelbu kula makombo (alama 12)

i. Wanasaamoyo wanafungiwa **soko** ambalo lilikuwa tegemeo adimu kwao;
ii. Wanasagamoyo wanapandishiwa **bei** ya bidhaa katika kioski ya soko;
iii. Vijana **wanauawa** wakati wa migomo;

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

iv. Wanasaga wanafungiwa **vyombo** vya habari na mitandao ya kijamii;
v. Wanasaga wanarushiwa **vijikaratasi** ili wahame Saga, mfano Siti na Kombe;
vi. Walimu na madaktari wanaongezewa mshahara na kupandishiwa **kodi**;
vii. Majoka ananyakua ardhi ya Wasaga na kujenga hoteli ya kifahari;
viii. Majoka anawaaawia vikaragosi wake ardhi ya Wanasaga mfano Kenga.
ix. Majoka anafungulia biashara ya ukataji **miti** na kuwafanya Wasaga kukosa maji kwa sababu mito na maziwa imekauka;
x. Wanasagamoyo wanakufa na kupofuka kutokana na kubugia **pombe** haramu aliyoigema Asiya baada ya kupewa kibali kuigema;
xi. Majoka anawatuma **wahuni** kumuumiza na kumvunja muundi Tunu;
xii. Majoka anaagiza **Ngurumo** azikwe juu ya miili mingine akidai kimba ni kimba tu;
xiii. Wanafunzi katika shule ya Majoka wanadungwa sumu ya nyoka na kuwa **makabeji**;
xiv. **Ashua** anafungwa bila hatia;
xv. Wanasagamoyo wanaomfanyia kazi katika Majoka katika kampuni yake hawalipiwi **bima**;
xvi. Majoka anawa**tusi** Wasaga wanapokataa kwenda mkutano wake ikuluni;
xvii. Majoka kuwakutanisha Ashua na Husda na kuwapiganisha katika ofisi yaumma.

***Mwanafunzi aonyeshe jinsi Wanasagamoyo wameteseka , wamedharauliwa, kukandamizwa au kudhalilishwa.***

*(zozote 12x1=alama 12)*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU D**

**Hadithi Fupi:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* - Chokocho Na D. Kayanda:

Jibu swali la *6* au *7*

**6.**

i) Tathmini umuhimu wa Samueli Matandiko  Katika kuijenga hadithi, “Mtihani wa Maisha”
(alama 10)

i. Samueli anachimuza maudhui  ya **elimu**,anaendea matokeo yake shule yakushtua;
ii. Anaendeleza maudhui ya **ubabedume**,kupitia kwake baba haoni umuhimu wa kumfunza;
iii. Anajenga maudhui ya **ndoa** au familia,wazazi wake wanampa elimu sawa na dadazake;
iv. Samueli anachimuza maudhui ya ya **bidii** kwenye hadithi.aliamka asubuhi na kutembea kilomita sita hadi shuleni na kurudi;
v. Samueli anajenga sifa za **wahusika** wegine,mfano mama ni mwenye ukarimu,upendo;

vi. Anasuka **ploti** kwa kudokeza walikofumea mwajuma na hivyo kubadilisha mkondo wa usimulizi;
vii. Kupitia kwa Samueli tunaona baadi ya wanafunzi wanajihusisha na **mizaha** wakiwa shuleni jambo ambalo linapelekea kufuli kwao;
viii. Samueli anajihusisha na mahusiano akiwa shuleni,Nina ni mpenzi wake;
ix. Babake Samueli **anawajibikia** familia yake kwa kulipia Samueli na dadake karo;
x. Sifa ya uwajibikaji imejitokeza kwa mama samueli anapompikia **chakula** na kumpa chajio.

*(zozote 10x1= alama 10)*

ii) Fafanua shibe inavyomaliza Waafrika katika hadithi ya "Shibe Inatumaliza". (alama 10)

i) Magonjwa kama presha, *obesity*, saratani yanawakumba kutokana na uongozi mbaya;
ii) Kuuwana kwa mabomu, risasi, kunyongana;
iii) Mzee Mambo kutumia **runinga** ya Taifa kutangaza sherehe yake ya binafsi;
iv) Dj kupata huduma za **kimsingi** kama maji ilhali wananchi hawana;
v) Dj anatumia sherehe ku**chota** mabilioni ya pesa pzmoja na viongozi wengine;
vi) Sasa na Mbura, ni mawaziri wawili wa **wizara** moja ya Mipango na Mipangilio;
vii) Mzee Mambo kupokea **mshahara** ilhali hafanyi kazi yoyote;
viii) **Magari** ya umma kubeba jamaa wa Mambo;
ix) **Chakula** cha sherehe kinapikiwa ikulu;
x) Ukoloni mamboleo- mchele wa basmati;
xi) **Dj** kumiliki duka la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kuu;

*(zozote 5x2=alama 10)*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

"Tulipokutana Tena" - Alifa Chokocho

**7.** ***a)*** 'Jijini ni kuzuri. Kuna majumba makubwa, utapanda magari mazuri mazuri ya marafiki zetu, utakula vyakula vitamu na kupewa nguo za fahari. Utapelekwa shule kusoma na kwandika.'

i) Jadili muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

i) Haya msemaji ni **Babake** Bogoa;
ii) Wanaoambiwa ni kina **Sebu**, Kazu,Temu, Tunu na Sakina;
iii) Wako ***Club** Pogopogo;*
iv) Bogoa anawasimulia kadhia iiliyowa**fika** anapotolewa kwao.

*(zote 4x1=alama4)*

ii) Eleza taswira zinazojitokeza katika dondoo hili kwa kutoa mifano. (alama 3)

i. Taswira **oni**: majumba makubwa makubwa;
ii. Taswira **mwonjo**: utakula vyakula vitamu;
iii. Taswira **mwendo**: utapelekwa shule…

*(zozote 3x1=alama 3)*

iii) Aliyoambiwa msemewa ni kinyume cha yaliyotokea. Eleza. (alama 8)

**Masaibu ya Bogoa**

i. Kula kutoka kwa **vigae**/sufuria wengine wakila kwa sahani;
ii. Kuchomwa kwa kijinga alipokuwa akioka maandazi aka**lala** yakaungua;
iii. Kukatazwa asiende kwa **shule** kama watoto wengine;
iv. Kunyimwa **ushirika** na watoto wa Bi Sinai, wasicheze pamoja;
v. Kukatazwa asiende kwa kina Sebu **kucheza**;
vi. Ku**fanyishwa** kazi ngumu kama kuchanja kuni, kuteka maji, kufua;
vii. **Kuchapwa** sana alipochelewa kurudi;
viii. Kutishiwa kukatwa **ulimi** iwapo angesema kwa yeyote yaliyojiri humo nyumbani;
ix. Kunyimwa ushirika na **wazazi** wake walipokuja kumwona;
x. Kulazimika **kuamka** mapema akiwa mtoto mdogo;
xi. Kula makoko ya vyakula au makombo.

*(zozote 8x1= alama 8)*

***b)*** Wahusika mbalimbali katika hadithi hii wanatumia njia nyingi kukabiliana na matatizo yanayowakumba. Zijadili.

(alama 5)

i. Bogoa anapelekwa ku**lelewa** na Bi Sinai kwa sababu ya umaskini;
ii. Bogoa kuweka **siri** ya kutoroka kwake hata hakumwambia rafikiye Sebu;
iii. **Kuhama** kwa Bi Sinai kwa Bogoa ni njia moja anakabiliana na tatizo;
iv. Bogoa kumwaga **dukuduku** lake kwa kuwahadithia marafiki wake yale yaliyomfika kwa Sinai;
v. Bogoa kutia **bidii** katika maisha kwa sababu yeye ni sonara huko Tinya;
vi. Bogoa alioa Sakina ili amwondolee upweke huko Tinya;
vii. **Kusamehe** wazazi wake na mlezi wake Bi Sinai;
viii. Sebu na mkewe Tunu wanatembelea **marafiki** zao, Kazu na Temu ili kuongea,

*(zozote 5x1 =alama 5)*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**SEHEMU YA E**

**Fasihi Simulizi**

Malaika …..

Nakupenda malaika x 2

Ningekuoa mali we…..

Ningekuoa dada…..

Nashindwa na mali sina we…..

Ningekuoa malaika x 2

Pesa, zasumbua roho yangu x 2

Nami nifanyeje, kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina we

Ningekuoa malaika x 2

i. Tambua utungo huu. (alama 2)
**Wimbo** au
Wimbo wa mapenzi
*(Hoja 1x2=alama2)*

ii. Toa sababu za jibu lako hapo juu (alama 2)
   i. Matumizi ya **lugha** ya mkato na ya kuvuta: mali we…
   ii. **Urudiaji** wa vipande: ningekuoa malaika x2
   iii. Uwepo wa **beti**
   iv. Kuna **kiitikio**

*(Zozote 2x2=alama 4)*

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

iii. Taja shughuli ya kijamii na shughuli ya kiuchumi inayodokezwa kwenye kipera hiki. (alama 2)

i. Shughuli ya kijamii: kuoa/**ndoa**
ii. Shughuli ya kiuchumi: ulipaji **mahari**

*(Zote 2x1=alama2)*

iv. Tambua nafsi neni na nafsi nenewa. (alama 2)
Nafsineni: **kijana** anayetaka kuoa
Nafsinenewa: **msichana** anayechumbiwa.

v. Jadili vipi mwasilishaji wa kipera hiki anaweza kuboresha wasilisho lake.(alama 6)

i. **Kupandisha** na kushusha sauti;
ii. Matumizi ya **viziada** lugha;
iii. Uwa **mfaraguzi**;
iv. **Kubadilisha** kiimbo na toni kulingana na hali;

v. Awe **jasiri** ili aweze kuimba bila aibu;atumie maleba yafaayo kuwasilisha ujumbe

*(zozote 3x2=alama 6)*

vi. Ni matatizo yapi yanayoweza kumkumbuka mkusanyaji wa kipera hiki nyanjani? (alama 6)

i) **Gharama** za utafiti ni ghali, mfano kununua vifaa kama tepurekoa;
ii) Kupotea au kufisidiwa **vifaa** vya kuhifahi data;
iii) Ukosefu wa **wakati** wa kutosha wa kufanyia utafiti;
iv) Vikwazo kutoka kwa **watawala** – kunyimwa nafasi;
v) Matatizo ya **mawasiliano** na uchukuzi – magari;
vi) Matatizo ya kibinafsi mfano kushinwa kudhibiti **wahojiwa**;
vii) Ukosefu wa **usalama**, mfano kuvamiwa.

*(zozote 2x3=alama6)*

***MWISHO***

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources